(k) Kutumia njia ya usambazaji wa maji ya umwagiliaji kwenye mimea katika ardhi yake ambayo haijapata kibali cha Tume.

**4. Mambo yanayotarajiwa katika Usimamizi wa Sheria**

Kutokana na hali iliyokuwepo na changamoto ambazo zimeikabili sekta ya umwagiliaji kwa muda mrefu, baadhi ya mambo yafuatayo yanatarajiwa kwa uwepo wa Sheria hii:

(a) Kuongezeka kwa mchango wa umwagiliaji katika uzalishaji wa chakula na lishe;

(b) Kuongezeka kwa pato la wakulima wamwagiliaji na Taifa kwa ujumla kwa kuwa skimu zitakuwa na usimamizi mzuri;

(c) Kuongezeka kwa fursa za ajira na kipato kwa vijana kutokana na vivutio katika kilimo cha umwagiliaji na hivyo kupunguza wimbi la vijana kukimbilia mijini.

(d) Kuongezeka kwa miundombinu ya umwagiliaji yenye ubora itakayotumia teknolojia mbalimbali kutokana na ushiriki mzuri wa sekta ya umma na binafsi;

(e) Kupata teknolojia mpya za kilimo cha umwagiliaji kutokana na shughuli za utafiti wa umwagiliaji kupata msukumo kisheria.

(f) Kuwepo kwa skimu nyingi za umwagiliaji zenye kutumia rasilimali maji na ardhi kwa ufanisi na kuzingatia hifadhi ya mazingira.

(g) Uwepo wa vyama imara vya wamwagiliaji vyenye stadi stahiki katika usimamizi wa skimu za umwagiliaji na hivyo kuwa na miundombinu ya umwagiliaji inayotumiwa vizuri.

**UMWAGILIAJI NI KILIMO CHA UHAKIKA**



Banio la kisasa - Skimu ya Umwagiliaji Ndungu (Kilimanjaro)

Ongezeko la mavuno ya mpunga hadi tani 8-10 kwa hekta



*Kwa maelezo zaidi wasiliana na:*


**MKURUGENZI MKUU**

**TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI**

**S.L.P. 146**

**DODOMA**

*e-mail:* **info@nirc.go.tz**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI**

# IJUE SHERIA YA TAIFA YA UMWAGILIAJI NA. 4 YA MWAKA 2013

## 1. Utangulizi

Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na. 4 ya mwaka 2013 imetungwa na kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2013, ikatiwa saini na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Oktoba 2013. Sheria hii imeanzisha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji; kwa anilid ya Kusimamia kilimo cha Umwagiliaji Nchini.

Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji ilitungwa ili kuondoa changamoto zilizokuwa zinaikabili Sekta ya Umwagiliaji, kama ifuatavyo:

- Ushiriki mdogo wa wakulima na sekta binafsi katika ujenzi, usimamizi na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji ambazo hujengwa na serikali kwa fedha nyingi, hali hii ilisababishwa na kutokuwepo wajibu wa kisheria wa wakulima kuchangia mipango ya kuendeleza sekta ndogo ya umwagiliaji hata kupelekea dhana kwa wakulima kuona kuwa miundombinu hiyo siyo mali yao.
- Udhaifu wa mfumo wa kitaasisi ambao ulikuwa haukidhi kasi ya kuendelea kupanuka kwa mahitaji ya kilimo cha umwagiliaji kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na kupungua kwa mvua, hivyo kufanya watu wengi kuingia kwenye kilimo cha umwagiliaji.
- Uvamizi wa maeneo ya ardhi yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji kwa matumizi mengine yakiwemo makazi. Hali hii ilisababishwa na kutokuwepo na mfumo wa kisheria wenye kulinda na kuendeleza ardhi inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ili isivamiwe kwa matumizi mengine hasa ukizingatia kuwa Taifa linahitaji kujitosheleza kwa chakula hasa katika kipindi hiki cha mabadiliko ya tabia nchi.

## 2. Mambo muhimu yanayozingatiwa katika Sheria

(a) Uanzishwaji wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Kifungu cha 3(1) na (2) na kifungu cha 5(1) na (2). Cha Sheria ya umwagiliaji kinabainisha Mamlaka na Majukumu yake.

(b) Kifungu cha 5(2)(c) cha Sheria ya Umwagiliaji kimeonesha Mfumo wa kisheria kuhimiza na kuvutia ushiriki wa wadau mbalimbali katika sekta ya umwagiliaji.

(c) kifungu cha 12(1)- (7).cha Sheria ya Umwagiliaji kinaipa Mamlaka Serikali za Mitaa katika uendelezaji na usimamizi wa skimu za umwagiliaji.

(d) Majukumu ya vyama vya wamwagiliaji yamebainishwa katika kifungu cha 31 cha Sheria ya umwagiliaji kama ifuatavyo;

(i)Kusimamia Uendeshaji na Matunzo ya Miundo mbinu ya Umwagiliaji

(ii) Kusimamia upatikanaji Maji ya Kutosha Kwenye Vitalu na Maandalizi mazuri ya Kalenda ya msimu wa kilimo

(iii) Kusimamia matumizi bora ya maji.

(iv) Kutunza daftari la wanachama wa Umwagiliaji katika skimu.

(v) Kusimamia na kuweka rekodi za mtiririko wa maji kwa ajili ya umwagiliaji.

(vi) Kutatua matatizo katika skimu kwa wanachama

(vii) Kuhakikisha Ukaguzi wa hesabu za mwaka unafanyika na taarifa nyingine za kihesabu .

(viii) Kuandaa na kutunza mali na madeni katika Skimu za umwagiliaji.

(e) Kifungu cha 32 Cha Sheria ya umwagiliaji Kimebainisha vyanzo vya fedha katika vyama vya umwagiliaji ambavyo ;

(i)Ada ya Uanachama,

(ii) fedha za misaada kutoka Serikalini au sekta binafsi.

(f) Kifungu cha 20 (1)- (5) cha Sheria ya umwagiliaji kimetoa utaratibu wa kuomba, kuidhinisha na kutekeleza ujenzi wa Miundombinu ya umwagiliaji.

(g) Kifungu cha 52(1) na (2). Cha Sheria ya umwagiliaji kimeeleza uanzishwaji,utaratibu na Usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji.

(h) Kifungu cha 59(1) na (2) cha Sheria ya umwagiliaji kimeweka utaratibu wa Tume kupata fedha kwa njia ya mikopo na misaada kutoka katika taasisi za fedha kwa ajili ya kuendeleza umwagiliaji.).

(i) kifungu cha 13(1) - (5) cha Sheria ya umwagiliaji iimeelekeza vyama vya umwagiliaji kuwa na wakaguzi wa kwa ajili ya kukagua mapato na matumizi.

(j) kifungu cha 67(1) - (3) cha Sheria ya umwagiliaji kinatoa fursa kwa Jukwaa la wadau kujadili masuala ya umwagiliaji

(k) Makosa na adhabu yamebainishwa katika Vifungu vya 61(1) - (5) na 62(1), na (2) vya Sheria ya umwagiliaji.

(l) kifungu cha 51(1) - (3) cha Sheria ya umwagiliaji kineeleza jinsi ya Kusimamia na kuendeleza Tafiti katika umwagiliaji .

(l )Utaratibu wa kukusanya ada ya Umwagiliaji umebainishwa katika kifungu cha 39(1) na (2). Ambapo Tume au Mamlaka ya Serikali za mitaa au vyama vya umwagiliaji zitasimamia ukusanyaji wa ada na tozo.

## 3. Vitendo vilivyokatazwa katika Sheria

Kifungu cha 45(1) kimebainisha kuwa itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya yafuatayo:-

(a) Kutumia au kuingia katika ardhi ya umwagiliaji kwa madhumuni mengine zaidi ya kilimo cha umwagiliaji;

(b) Kuruhusu sumu ya viwandani au uchafu wa nyumbani katika skimu yoyote ya umwagiliaji, bila kutibu maji kikamilifu;

(c) Kuzuia ufanisi wa maumbo mbalimbali ya mfumo wa matupio na kuhatarisha usalama wa mifereji ya kusafirisha maji ya umwagiliaji na matupio;

(d) Kufungua au kufunga mlango au chombo cha kudhibiti mwenendo wa mafuriko kwenye bwawa, mfereji au mfumo wowote wa kusafirisha maji kwenye miundombinu ya umwagiliaji unaomilikiwa na kuhudumiwa na Serikali au vyama vya wamwagiliaji isipokuwa Mkaguzi wa Umwagiliaji au mtu yeyote aliyepewa mamlaka hayo;

(e) Kuvua katika mabwawa yanayomilikiwa, kutunzwa au kusimamiwa na Serikali au vyama vya wamwagiliaji bila kibali cha maandishi kutoka kwa mkaguzi wa umwagiliaji isipokuwa kwa masharti na vigezo na kwa kulipa ada kama itakavyopangwa;

(f) Kutumia milipuko au kitu chochote cha sumu kwa madhumuni ya kuvua katika bwawa;

(g) Bila kibali cha maandishi cha Tume kuchimba madini au kufanya shughuli kwa kutumia mlipuko au shughuli yoyote inayoweza kusababisha mtikisiko ndani ya umbali wa kilometa moja kutoka kwenye skimu;

(h) Kuruhusu maji kutoka katika miundombinu ya umwagiliaji inayomilikiwa, kusimamiwa au kutunzwa na Serikali au vyama vya wamwagiliaji kwa kukata tuta au kutoboa, kujenga mlango au kwa njia nyingine zinazofanana na hizo;

(i) Kuunganisha mifereji au bomba kwenye mifumo ya umwagiliaji au matupio;

(j) Kuweka au kusababisha kuweka umbo au kuweka kifaa katika mfereji au bomba iliyounganishwa kwenye mifumo ya umwagiliaji na matupio; na